

Mpango wa Usaidizi wa Makazi

Mpango wa Usaidizi wa Makazi ni mpango wa huduma ya usaidizi wa makazi unaotoa usaidizi wa kifedha mara moja au kwa muda mfupikwa wanafamilia wanaokabiliana na matatizo ya makazi ya muda mfupi, yasiyo ya mara kwa mara. Wapangaji na wamiliki wa nyumba wa Jiji la Pittsburgh wanaweza kupokea hadi \$6,000 ya usaidizi wa makazi.



Usaidizi wa Mpango Wa:

- Usaidizi wa Kupanga Nyumba
 - Kodi ya mwezi wa kwanza
 - Kodi ya mwezi uliopita
 - Amana ya usalama
- Kodi
- Usaidizi wa kulipa rehani (ikiwa haipo katika Sheria ya 91)

Jumla ya kiwango cha juu zaidi cha usaidizi kwa wapangaji na wamiliki wa nyumba ni \$6,000.

Waombaji wanaweza kuomba usaidizi wa mpango mara moja kila baada ya miaka 3.

Mahitaji ya Kustahiki:

- Lazima uwe mpangaji au mmiliki wa nyumba anayeishi ndani ya mipaka ya Jiji la Pittsburgh
- Wapangaji lazima wawe na kiwango cha mapato cha au chini ya 50% ya Mapato ya Wastani ya Eneo (AMI) na wamiliki wa nyumba lazima wawe na kiwango cha au chini ya 80% ya AMI (Angalia chati iliyo upande wa kulia).

Viwango vya Juu Zaidi vya Mapato:

Chati hii inaonyesha viwango vya juu zaidi vya mapato ya kila mwaka vya Mpango wa Usaidizi wa Makazi. Mapato kwa Jumla ya Mwaka = Jumla ya mapato ya wanafamilia wote, kabla ya ushuru na kodi ya zuio

Idadi ya Wanafamilia	Kiwango cha juu zaidi cha Mapato kwa <u>WAPANGAJI</u>	Kiwango cha juu zaidi cha Mapato kwa <u>WAMILIKI WA NYUMBA</u>
1	\$35,150	\$56,250
2	\$40,200	\$64,250
3	\$45,200	\$72,300
4	\$50,200	\$80,300
5	\$54,250	\$86,750
6	\$58,250	\$93,150
7	\$62,250	\$99,600
8	\$66,300	\$106,000

Tazama ukurasa wa nyuma wa kipeperushi

Jinsi ya Kutuma Ombi

Kabla ya kutuma ombi la usaidizi, kusanya hati zifuatazo zinazohitajika ili utume ombi:

- Uthibitisho wa mapato: W-2, karatasi za mshahara na makato yake, barua ya misaada ya kutokuwa na ajira, au barua kutoka kwa mwajiri
- Uthibitisho kuwa unahitaji msaada: Notisi ya kuchelewa kulipa kodi au notisi ya kufukuzwa kutoka kwa nyumba

Tuma Ombi la Usaidizi wa Kupanga Nyumba au Kulipa Kodi:



Piga simu kwa [412-248-0021](tel:412-248-0021) ili ufanyiwe tathmini ya kuona ikiwa unastahiki kwa usaidizi wa kulipa kodi au kupanga nyumba. Huduma za simu ni za bure na za siri. Huduma za lugha za tafsiri na ukalimani zinapatikana.



Tuma barua pepe kwa rentalassistance@actionhousing.org.

Tuma Ombi la Usaidizi wa Kulipa Rehani:



Allegheny Link



Piga simu kwa [1-866-730-2368](tel:1-866-730-2368) ili ufanyiwe tathmini ya kuona ikiwa unastahiki kwa usaidizi wa kulipa rehani. Huduma za simu ni za bure na za siri. Huduma za lugha za tafsiri na ukalimani zinapatikana.



Tembelea [415 Seventh Avenue, Pittsburgh, PA 15219](#), ambayo hufunguliwa Jumatatu - Alhamisi kuanzia saa 9:30 Asubuhi hadi saa 4:30 Jioni. Ikiwa unakwenda huko wewe binafsi, unapaswa kuleta hati zilizo rodheshwa juu ya ukurasa huu. Ingawa hazihitajiki, huenda ni vizuri pia kuleta kadi za usalama wa kijamii, vyeti vya kuzaliwa, na vitambulisho vya picha vya wanafamilia wote, pamoja na nakala halali ya mkataba wako wa kupangisha nyumba, kwa ajili ya kutumwa ili upate usaidizi wa mipango na rasilimali nyingine.